# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA

Baraza la Mitihani la Tanzania limesikitishwa na taarifa ya **UONGO** iliyotolewa na Gazeti la Nipashe toleo Na. 0579130 la tarehe **19 Februari 2017** yenye kichwa cha habari kilichosomeka **Mchujo FORM 1 Wasisitizwa**. Katika taarifa hiyo mwandishi aliuarifu umma kuwa Katibu Mtendaji amesisitiza uwepo wa Upimaji huo na kwamba umeshapitishwa. Baraza linapenda kuwajulisha wanafunzi na umma kwa ujumla kuwa taarifa hizo ni za **UONGO** na zinalenga kupotosha umma na kuleta taharuki.

Hivyo,Baraza linaomba umma kuzipuuza taarifa hizo kwa kuwa upimaji huo **ULISHASITISHWA** na **HAUTAKUWEPO**.

Imetolewana,

**AFISA HABARI NA UHUSIANO**